BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 25 Juni, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2018/2019.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

216. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hivi karibuni Serikali imeanza utekelezaji wa sera ya ugatuzi kwa sekta ya afya, elimu na kilimo katika hatua za msingi.

Jambo hili jema limeanza na changamoto kadhaa kutokana na kukosekana kwa miongozo ya utekelezaji tokea mwanzo.

Je, ni lini miongozo ya utekelezaji wa sera ya ugatuzi itapelekwa katika sekta husika ili kuondoa matatizo mbali mbali yanayojitokeza hivi sasa katika utekelezaji wa sera hiyo ya ugatuzi.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

257. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Katika kudumisha historia ya nchi na kukuza utalii na kuongeza mapato ya Taifa, yapo mambo ya kale na sehemu za makumbusho ambayo yanajulikana lakini bado hayajapewa kipaumbele katika matunzo na kuyalinda maeneo hayo ambapo mengine yameanza kuvamiwa, kuharibiwa na kupoteza uhalisia wake.

(a) Je, Wizara inafahamu maeneo yote ya kihistoria na sehemu za makumbusho na mambo ya kale yaliyopo Zanzibar.

(b) Je, maeneo hayo yamepimwa na kupewa hati.

(c) Je, maeneo hayo yanafaa kuwekewa uzio au hayafai, na kama yanafaa kwa nini hayaekewi uzio.

Wizara ya Elimu na MAfunzo ya Amali:

19. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje):- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Ukutini Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kukithiri vitendo vya utoro wa wanafunzi.

(a) Nini chanzo cha kukithiri kwa utoro katika Skuli hiyo.

(b) Je, hatua gani madhubuti zimechukuliwa kukabiliana na vitendo hivyo vya utoro.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

225. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Kwa kuwa michezo, utamaduni na sanaa, huitangaza nchi kwa fani hizo, na pia wanamichezo hujulikana nchi mbali mbali kwa fani zao hizo na kwa kuwa tuna wanamichezo mbali mbali nchini, ambao wameitangaza nchi yetu ndani na nje ya nchi.

Je, Wizara ina mpango gani wa kukutana nao wanamichezo hao.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

186. MHESHIMIWA ASHA ABDALLA MUSSA (Jimbo la Kiwengwa - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Wananchi wa Zanzibar asilimia 90 ni wakulima wa mpunga na unapofika wakati wa kilimo hutumia matrekta ya Serikali ambayo ni bei nafuu. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kubwa juu ya matrekta hayo hali inayowafanya wananchi hao kutumia gharama kubwa kutafuta matrekta binafsi au kukosa kulimiwa kwa wakati.

(a) Je, kwa Unguja na Pemba kuna matrekta mangapi ambayo yanafanya kazi.

(b) Je, ni lini tatizo hilo litaondoka ili wananchi waondokane na kadhia hiyo.

250. MHESHIMIWA ALI KHAMIS BAKAR (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Naipongeza Serikali kwa kuanzisha Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa ajili ya kusimamia na kuimarisha shughuli za matrekta na kilimo.

Na kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar alitoa agizo kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuupatia Wakala huu jumla ya

matrekta (20) kutoka Kampuni ya (Mahindra) ili kuzidi kuongeza nguvu kiutendaji na kuinua hali za wakulima wetu. Na kwa kuwa Wakala huu ulipokea jumla ya matrekta (10) mapya kutoka Ubalozi wa Libya ambayo yameshindwa kufanya kazi mara tu baada ya kufika kutokana na kutolewa baadhi ya vifaa huko yalipohifadhiwa.

(a) Je, ni lini vifaa hivyo vilivyoibiwa vitanunuliwa vipya ili matrekta hayo yatoe huduma kama ilivyokusudiwa.

(b) Wizara ya Fedha na Mipango ina mpango gani wa kuipatia fungu lake la matumizi (Vote) kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Wakala huu.

(c) Je, lini agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar litatekelezwa ili kufikia lengo na dhamira yake aliyoikusudia kwa kilimo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

65. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kumekuwa na kilio cha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuhusu Taasisi za Serikali ambazo zinachelewa kulipa madeni yao ya umeme kwa muda mrefu, tofauti na Taasisi binafsi na wananchi ambao wakichelewa kidogo tu wanakatiwa huduma hiyo ya umeme.

(a) Je, ni Taasisi zipi za Serikali ambazo ni wadaiwa sugu wa deni la umeme la ZECO.

(b) Kuna hatua gani kabambe za kudai madeni hayo.

(c) Kwanini Taasisi hizo hazikatiwi umeme zinapochelewa kulipa deni.

174. MHESHIMIWA ASHA ABDALLA MUSSA (Jimbo la Kiwengwa) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Imekuwa desturi kwa vituo vya maji safi na salama Unguja na Pemba mara kwa mara kuharibika pampu ambazo

matengenezo yake huchukuwa muda hadi kukamilika na kupelekea usumbufu kwa wananchi kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea kuharibika mara kwa mara mashine hizo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha tatizo hilo halijitokezi mara kwa mara.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

36. MHESHIMIWA ALI KHAMIS BAKAR (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Kitengo cha vipimo na mizani kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya Vipimo ya mwaka 1983, katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2017 kilifanya ukaguzi Unguja na Pemba na kilikusanya jumla ya Tshs. 23.7 milioni.

(a) Je, mligundua nini katika ziara hii ya ukaguzi.

(b) Je, Sheria namba 4 ya mwaka 1983 ambayo ni ya zamani, ni lini itafanyiwa marekebisho.

(c) Ni mara ngapi kwa mwezi Wizara inafanya ukaguzi ili kubaini bidhaa mbovu madukani na kukagua mizani hizo.

255. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2017/2018, Waziri alieleza kwamba mazungumzo yanaendelea kuona kwamba Kiwanda cha Soda na Kiwanda cha Nguo cha Cotex kuweza kuviendeleza na kurudi katika hali yake au kuweza kufanya uzalishaji mwengine.

(a) Je, Wizara imefikia hatua gani.

(b) Je, Wananchi wategemee nini juu ya viwanda hivyo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

222. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe Fuoni, wananchi wanaipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kuondoa tatizo la usafiri. Pamoja na neema hiyo, bado kuna matatizo mengi ya ajali zinazosababishwa na madereva wazembe.

(a) Je, Wizara yako imejipanga vipi kuliondoa tatizo la ajali, katika maeneo ya Meli Nne, Taveta, Kijitoupele, Mashine ya Maji na Kwandundu.

(b) Je Serikali ina mpango gani wa kuweka matuta mapana ambayo hayataleta usumbufu kwa wasafiri.

248. MHESHIMIWA ALI KHAMIS BAKAR (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kikosi cha Zimamoto na Uokoozi Uwanja wa Ndege kinakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa maji kwa ajili ya kuendeshea shughuli zake. Na kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitembelea eneo hilo na kuwataka wahusika wakuu kuweka miundombinu bora katika eneo hilo, na ahadi hiyo haijatekelezwa hadi leo.

(a) Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa.

(b) Je, hatuoni kufanya hivyo ni kurudisha nyuma juhudi za Serikali.

(c) Ni kiasi gani cha fedha kinahitajika kuondoa tatizo hilo.

Wizara ya Afya:

127. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Vyakula na vinywaji vinavyotoka nje vinaingizwa nchini na wafanyabiashara wadogo wadogo pengine bila ya “Agent”

na vitu hivyo vinatiliwa mashaka kuwa huleta madhara kwa mlaji au watumiaji na pengine husababisha madhara makubwa kiafya au kifo.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika vyakula na vinywaji vinavyoingizwa nchini bila ya "*Agent*."

(b) Je, mtumiaji akipata tatizo kwa vyakula na vinywaji vilivyoingizwa, mtumiaji atapata malipo ya matibabu kupitia wapi.

(c) Je, imeshawahi kutokea tatizo hilo na Wizara ililimaliza vipi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2018/2019 na Lijadili na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2018/2019

Zanzibar,
25 Juni, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.